



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**OFISI YA RAIS**  
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**  
**HALMASHAURI YA WILAYA YA CHALINZE**



(Barua zote zilandikwe kwa Mkurugenzi Mtendaji)

*Unapojibu tafadhali taja:*

**Kumb. Na.HWC/S.30/29 VOL1/23**

**01/06/2023**

Wananchi Wote,  
**TANZANIA.**

**YAH: TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Chalinze anapenda kuwatangazia Watanzania wote kuwa, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kupitia barua yake yenye Kumb.Na.FA.97/228/01"TEMP"06 ya tarehe 06/04/2023 imetoa Idhini ya kutangaza na kuajiri nafasi za kazi za masharti ya kudumu kwa Halmashauri ya Chalinze zilizoidhinishwa kupitia bajeti ya mwaka wa fedha 2022/2023. Hivyo, watanzania wote wenye sifa mnakaribishwa kuomba nafasi hizo kama ifuatavyo;

**A: MSAIDIZI WA KUMBUKUMBU DARAJA LA II (RECORDS MANAGEMENT ASSISTANT II) – NAFASI 1**

**1. SIFA ZA MWOMBAJI**

- i. Awe amehitimu na kufaulu kidato cha nne (IV) au Kidato cha sita (VI).
- ii. Awe amehitimu Stashahada/Diploma katika fani ya Masjara katika vyuo vinavyotambulika na Serikali.

**2. MAJUKUMU YA KAZI**

- i. Kuorodhesha barua zinazoingia Masjara kwenye Regista (Incoming Correspondence Register).
- ii. Kuorodhesha barua zinazotoka nje ya taasisi (Outgoing Correspondence Register).
- iii. Kusambaza Majalada kwa watendaji (Action Officers).
- iv. Kupokea Majalada yanayorudi Masjara toka kwa watendaji.
- v. Kutafuta Kumbukumbu/Nyaraka/ Majalada yanayohitajika na watendaji.
- vi. Kurudisha Majalada kwenye shubaka/kabati la majalada (racks/filing cabinets) au mahali pengine yanapohifadhiwa.
- vii. Kufuatilia mzunguko wa majalada ndani ya taasisi (file tracking).

**3. NGAZI YA MSHAHARA**

- i. Ngazi ya mshahara ni TGS C<sub>1</sub> kwa mwezi.

## B. MASHARTI YA UJUMLA (MUHIMU YAZINGATIWE)

- i. Awe mtanzania mwenye umri kuanzia miaka 18 hadi 45.
- ii. Maombi yote yatumwe na nakala za vyeti vya Elimu ya Kidato cha nne (IV) / Sita (VI), vya taaluma na cheti cha kuzaliwa. Nakala za vyeti vithibitishwe na mahakama au mwanasheria aliyeidhinishwa au kutambulika na serikali.
- iii. Testimonials "Provisional Results", Statement of Results, Hati za matokeo kidato cha nne na sita HAVITAKUBALIWA.
- iv. Barua za maombi ziambatane na nakala za kitambulisho cha Taifa au namba ya kitambulisho cha Taifa.
- v. Waombaji waliosoma nje ya nchi ya Tanzania wahakikishe kuwa, vyeti vyao vimehakikikwa na kuidhinishwa na mamlaka ya NACTE, NECTA au TCU.
- vi. Watumishi wote waliowahi kufanya kazi katika utumishi wa Umma wakaacha kazi, kustaafu, wakastaafishwa, kufukuzwa kazi hawaruhusiwi kuomba isipokuwa kama wana kibali cha Katibu Mkuu (UTUMISHI).
- vii. Vyeti vyote vitafanyiwa uhakiki kwa kushirikiana na mamlaka husika NECTA na TCU.
- viii. Waombaji ambao tayari ni waajiriwa katika nafasi za kuingillia katika Utumishi wa Umma, wasiombe na wanatakiwa kuzingatia maelekezo yaliyo katika waraka wenye Kumb.Na.CAC.45/25/257/91//D/140 wa tarehe 30Novemba, 2010.
- ix. Waombaji wote waambatanishe passport size (picture) nne za rangi za hivi karibuni.
- x. Watakaofaulu kuitwa kwenye usaili, Majina yao yatawekwa kwenye Tovuti ya Halmashauri ya Chalinze yaani; [www.chalinzedc.go.tz](http://www.chalinzedc.go.tz).
- xi. Maombi yaambatanishwe na maelezo Binafsi (cv) na kutumwa kwa njia posta na sio vinginevyo.
- xii. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 14/06/2023 saa tisa (9:30) Alasiri.

Tangazo hili linapatikana pia katika Tovuti ya Sekretarieti ya Ajira [www.ajira.go.tz](http://www.ajira.go.tz) na katika Tovuti ya Halmashauri [www.chalinzedc.go.tz](http://www.chalinzedc.go.tz).

Maombi yote yatumwe kuptia posta tu kwa Anuani ifuatavyo:

MKURUGENZI MTENDAJI,  
HALMASHAURI YA CHALINZE,  
S.L.P.65,  
CHALINZE.

  
06/06/2023  
Archanus A. Kilaja  
KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI (W)  
CHALINZE.

